



TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI)

KIJUE KITUO CHA UTAFITI WA KILIMO TARI DAKAWA



KUANZISHWA KWA KITUO

Kituo Kilianzishwa Rasmi Mnamo Mwaka 1984 kwa Ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya watu wa Korea.

MAONO YA KITUO

Kuwa Kituo Kiongozi na Mahiri Katika Nyanja Ya Utafiti na Usambazaji wa Teknolojia za Kilimo katika Ukanda wa Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika.

DHIMA

Kuendeleza Na Kusambaza Matokeo Ya Utafiti Wa Zao La Mpunga, Mahindi Na Mbogamboga Yatakayoongeza Ufanisi Na Ustahimilivu Wa Mfumo Wa Kilimo dhidi ya Mabadiliko ya Tabia Nchi Ili Kuongeza Tija, Kuboresha Lishe Na Kuongeza Kipato cha Mkulima Huku Ikipunguza Matumizi ya Viuatilifu Na Mbolea Ili Kulinda Na Kuimarisha Maliasili.

SHUGHULI ZA KITUO

- Kufanya Utafiti Wa Mpunga, Mahindi, Mbogamboga (na Mazao Mengine kwa Kushirikiana na Vituo Vingine) Kwenye Maeneo Ya Nyanda Za Chini Na Juu Nchini
- Kuhakikisha Mafanikio Ya Utafiti (Teknolojia zilizogunduliwa) Yanasambazwa Kwa Wakulima na Wadau Wengine Ndani na Nje ya Nchi.



UTAFITI NA HUDUMA ZITOLEWAZO NA KITUO

- Utafiti wa ugunduzi wa mbegu bora za mazao mbalimbali ikiwemo mpunga, mahindi na mbogamboga
- Utafiti wa mbinu za utunzaji wa mazao shambani (Agronomic management packages)
- Utafiti wa mbinu za udhibiti wa wadudu na magonjwa sumbufu kwenye mazao hususani mpunga
- Ubunifu na usambazaji wa teknolojia kwa wadau wakiwemo wakulima ili kuongeza tija kwenye kilimo
- Ushauri wa mbinu bora za kutunza, kuhifadhi na kuongeza thamani ya mazao hasahasa zao la mpunga

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Meneja wa Kituo
TARI Dakawa**

S.L.P 1892, Morogoro, Tanzania

Simu: (+255) 23 2934300, Barua pepe: cmdakawa@tari.go.tz